# HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI YA CHUO KWENYE SHEREHE YA UFUNGUZI WA MAADHIMISHO YA MIAKA 50 YA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE TAREHE 29 JULAI, 2011

Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba,
**Waziri Mkuu Mstaafu;**

Mheshimiwa Frederick Sumaye,
**Waziri Mkuu Mstaafu;**

**Waheshimiwa Wajumbe wa Bodi ya Chuo,**

**Ndugu Mkuu wa Chuo;**

**Ndugu Wakuu wa Vyuo Wastaafu;**

**Waheshimiwa Viongozi wa Vyama vya Siasa,**

**Waheshimiwa Viongozi wa Dini;**

**Ndugu Wafanyakazi wa Chuo;**

**Ndugu Wanachuo;**

**Wageni Waalikwa;**

**Mabibi na Mabwana.**

Leo ni siku ya kihistoria kwa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere. Ni siku ambayo tunaadhimisha miaka hamsini ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere.

Chuo cha Kivukoni kilianzishwa rasmi tarehe 29 Julai, 1961 na kuzinduliwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyekuwa Waziri Mkuu akiongoza Serikali ya Ndani ya Tanganyika. Wazo la kuanzisha

Chuo kwa ajili ya kuwaandaa viongozi wa kushika madaraka katika Serikali ya Tanganyika huru lilikuwa ni la TANU. Katika Mkutano wake Mkuu wa Tabora wa mwaka 1958, TANU aliamua kuanzisha Chuo cha Watu Wazima aina ya Chuo cha Ruskin cha Uingereza. Wananchi na makampuni binafsi yalitoa mchango wao ambao uliwezesha "The Tanganyika Education Trust Fund" kununua Hoteli ya Ghana ambapo Chuo cha Kivukoni kilianzia. Chuo kilisajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 ikiwa ni kampuni binafsi iliyomilikiwa na "The Tanganyika Education Trust Fund", "The Tanganyika African National Union (TANU)", "The Tanganyika Federation of Labour (TFL)" na "The Cooperative Union of Tanganyika (CUT)".

Mwaka 1971 Chuo cha Kivukoni kilipewa majukumu mapya na TANU. Chimbuko la majukumu hayo ni Siasa ya Ujamaa na Kujitegemea na Sera ya Chama kushika hatamu za Uongozi. Majukumu hayo mapya yalikuwa ni pamoja na Chuo kufundisha itikadi ya Chama ya Ujamaa na Kujitegemea. Katika awamu hii ya pili Chuo kilijulikana kwa jina la Chuo cha Chama Kivukoni.

Kwa kuzingatia mahitaji ya mafunzo ya itikadi, Chuo cha Chama Kivukoni kilianzisha Vyuo vya Kanda 08: Mahiwa, Msaginya, Ilonga, Lushoto, Hombolo, Murutunguru, Kihinga na Zanzibar. Mafunzo ya itikadi yaligawanyika katika sehemu tatu: Mafunzo ya ulinzi (People's Combat), mafunzo ya nadharia ya darasani na mafunzo kwa vitendo katika Wizara na Idara za Serikali, Mashirika ya Umma na Vijiji vya Ujamaa.

Itakumbukwa kwamba tarehe 01 Julai, 1992 Nchi yetu ilirejea kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa. Kwa kuzingatia hali mpya ya kisiasa, Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM katika Mkutano wake wa Machi, 1992 iliamua kufunga na kuvikabidhi Serikalini Vyuo vyake vya Kanda isipokuwa Chuo cha Kanda cha Zanzibar. Aidha, Halmashauri Kuu ya Taifa iliamua kwamba Chuo cha Chama Kivukoni kitoe mafunzo ya taaluma katika Sayansi Jamii badala ya mafunzo ya itikadi.

Ili kukidhi mabadiliko hayo, Chuo kilisajiliwa upya chini ya Sheria ya Makampuni, Sura 212 tarehe 20 Novemba, 1992 kwa jina la Chuo cha Sayansi Jamii Kivukoni. Programu za mafunzo zilizoendeshwa na Chuo ni Cheti katika Kazi za Vijana, Stashahada ya Taaluma za Kijamii, Stashahada ya Masuala ya Jinsia katika Maendeleo na Stashahada ya Uchumi katika Maendeleo. Licha ya kuendesha programu za mafunzo ya kitaaluma, Chuo cha Sayansi ya Jamii Kivukoni kilikuwa na majukumu ya kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa sekta ya umma na sekta binafsi. Shughuli za Chuo cha Sayansi Jamii Kivukoni zilifikia tamati tarehe 30 Septemba, 2005.

Nafasi ya Chuo cha Sayansi Jamii Kivukoni ilichukuliwa na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ambacho kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 6 ya Mwaka 2005. Kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Namba 433 la tarehe 23 Desemba, 2005 Sheria hiyo ilianza rasmi kufanya kazi tarehe 01 Oktoba, 2005.

Tofauti na awamu tatu zilizopita, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kinamilikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara yenye dhamana ya Elimu ya Juu. Chuo kilipewa jina la

Mwalimu Nyerere kwa kutambua mchango wake katika kuasisi Chuo cha Kivukoni na katika harakati za ukombozi wa Nchi yetu na Afrika kwa ujumla.

Majukumu makuu ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere ni pamoja na haya yafuatayo:-

(1) Kuendesha mafunzo ya kitaaluma katika fani ya Sayansi Jamii kwa Kiwango cha Cheti, Stashahada na Shahada;

(2) Kufanya Utafiti;

(3) Kutoa ushauri wa kitaalamu;

(4) Kutoa huduma kwa umma.

Chuo kimesajiliwa na kimepatiwa ithibati na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Wakati tunaadhimisha miaka 50 ya Chuo, changamoto kubwa inayokikabili Chuo ni kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia maadili ya muasisi wa Chuo, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kwa kufanya hivyo, Chuo kitakuwa kinamuenzi Mwalimu Nyerere kwa vitendo. Aidha, Chuo kinakabiliwa na changamoto ya kuandaa viongozi wa Taifa letu hasa katika kipindi hiki cha mfumo wa vyama vingi vya siasa. Maandalizi ya viongozi ni muhimu katika kulinda maslahi ya Taifa.

Kwa makusudi nimeamua kutozungumzia mchango wa Chuo hiki katika maendeleo ya Taifa letu. Nimefanya hivyo kwa sababu baada ya ufunguzi kuna mdahalo ambao utajikita katika kujadili mchango wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika maendeleo ya Taifa letu kuanzia mwaka 1961 hadi 2005. Ni matarajio yangu kwamba kila mmoja

wetu atafaidika na mdahalo wa leo ambao utaongozwa na Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba, Waziri Mkuu Mstaafu.

Baada ya hotuba hii fupi, naomba sasa nitamke rasmi kwamba maadhimisho ya miaka 50 ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere yamefunguliwa.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

Salim Ahmed Salim
**MWENYEKITI WA BODI YA CHUO.**